FUNZO LA 42

1. Ingawaje miaka mingi ilipita tangu Mungu aahidi kumtuma Mwokozi, je, Mungu alisahau ahadi yake?
-La.

2. Je, Mungu aliwapa nani Ujumbe wake kuhusu kuja kwa Mwokozi?
-Manabii.

3. Je, ujumbe ambao Mungu aliwapa manabii kuhusu kuja kwa Mwokozi uliandikwa wapi?
-Katika kitabu cha Mungu, Biblia.

4. Je, Waisraeli wengi waliwasikiliza manabii wa Mungu?
-La.

5. Je, Waisraeli waliwafanyia nini manabii wa Mungu?
-Waliwaua.

6. Badala ya kuwasikiliza manabii, je, Waisraeli walisikiliza nani?
-Manabii wa uongo.

7. Manabii wa uongo walikuwa wakisema kuwa walinena ukweli wa Mungu, lakini walinena nini?
-Uongo wa Shetani.

8. Je, Mungu alikubali ibada ya Waisraeli walioabudu mifano walioifanya na pia kumwabudu Mungu katika hekalu?



-La.

9. Je, kwa nini Mungu alikataa ibada ya Waisraeli walioabudu mifano walioifanya na kumwabudu Mungu pia hekaluni?
-Kwa sababu Mungu alijuwa kuwa walikuwa wakimwabudu kwa vinywa tu.
-Kwa sababu Mungu alijua kuwa waliabudu mifano kwa mioyo yao.

10. Je, ni nani ajuaye kila kitu mioyoni mwetu?
-Mungu.

11. Je, Mungu anasema nini kuhusu mioyo yetu yote?
-Mungu anasema kuwa mioyo yetu yote imejaa dhambi.

12. Ingawaje wengi wa Waisraeli waliabudu mifano, je, kuna baadhi yao ambao walimwabudu Mungu?
-Ndiyo. Kulikuwepo na wachache.

13. Je, hao Waisraeli waliomwabudu Mungu walimsubiri nani?
-Walisubiri Mungu amtume Mwokozi.

-Mungu ni mvumilivu.

-Mungu huwasubiri watu waache njia ya dhambi na wafuate njia ya Mungu.

-Mungu aliwasubiri watu wa wakati wa Nuhu miaka 120 ili waache njia ya dhambi na wafuate njia ya Mungu.

-Mungu pia aliwasubiri Waisraeli miaka 200 ili waache njia ya dhambi na wafuate njia ya Mungu.

-Lakini Waisraeli hawakuacha njia ya dhambi.

-Waisraeli walidhani kuwa Mungu angesahau dhambi yao.

-Je, Mungu alisahau dhambi yao?
-La.

-Waisraeli walifikiri kuwa Mungu hangeadhibu dhambi yao.

-Je, Mungu huadhibu dhambi yote?
-Ndiyo.

-Kama vile Mungu alivyoadhibu dhambi ya watu wa wakati wa Nuhu, ndivyo alivyoadhibu dhambi ya Waisraeli.

-Je, Mungu aliadhibu vipi makabila kumi ya Israeli?

-Mungu alituma Waasiria kuyashinda makabila kumi ya Israeli, Waasiria waliwafanya Waisraeli kuwa watumwa wao.

Tusome 2 Wafalme 17:5-8

5-Ndipo mfalme wa Ashuru akakwea katikati ya nchi
yote, akaenda Samaria, akauhusuru miaka mitatu.
6-Katika mwaka wa kenda wa Hoshea, huyo mfalme wa
Ashuru akautwaa Samaria, akawahamisha Israeli mpaka
Ashuru, akawaweka katika Hala na Habori, karibu na mto wa
Gozani, na katika miji ya Wamedi.
7-Yalitukia hayo kwa sababu wana wa Israeli walikuwa
wametenda dhambi juu ya Bwana, Mungu wao, aliyewaleta
kutoka katika nchi ya Misri watoke chini ya mkono wa Farao
mfalme wa Misri, wakawaacha miungu mingine.
8-Wakaziendea sheria za mataifa, ambao Bwana
aliwafukuza mbele ya wana wa Israeli, na sheria za wafalme wa
Israeli walizozifanya.



-Waasiri waliyashinda makabila kumi ya Israeli na kuwachukua wengi wao kwenda Asiri ili kuwafanya watumwa wao.

-Waasiri pia waliwaleta watu wengine kutoka nchi zingine ili waishi na Waisraeli waliosalia Israeli.

-Watu walioletwa kutoka nchi zingine hawakumwamini Mungu, bali waliabudu mifano walioifanya.

-Hao watu walikuwa Waisraeli waliosalia katika nchi ya Israeli, na uzao mpya wa watu ukaanza.

-Hawa watu wapya waliitwa Wasamaria.

-Wasamaria walimwabudu Mungu kwa njia yao wenyewe, bali si kwa njia ya Mungu.

-Baada ya Mungu kuadhibu makabila kumi ya Israeli, je, Mungu aliadhibu vipi makabila mawili ya Yuda?

-Mungu alituma Babeli kuyashinda makabila mawili ya Yuda,

Wababeli waliwafanya watumwa wao.

Tusome 2 Wafalme 25:1-7

1-Ikawa katika mwaka wa kenda wa kutawala kwake, katika mwezi wa kumi, na siku ya kumi ya mwezi huo, Nebukadreza, mfalme wa Babeli, akaja, yeye na jeshi lake lote, kupigana na Yerusalemu, akapanga hema zake kuukabili; nao wakajenga ngome juu yake pande zote.

2-Basi mji huo ulihusuriwa hata mwaka wa kumi na moja wa mfalme Sedekia.

3-Siku ya kenda ya mwezi wa nne njaa ilikuwa nzito ndani ya mji, hata hapakuwa na chakula kwa watu wa nchi.

4-Ndipo mahali pakabomolewa katika ukuta wa mji, watu wote wa vita wakakimbia usiku kwa njia ya lango lililokuwa kati ya zile kuta mbili, karibu na bustani ya mfalme; (basi wale Wakaldayo walikuwa wakiuzuia mji pande zote;) mfalme akaenda kwa njia ya Araba.

5-Lakini jeshi la Wakaldayo wakamfuatia mfalme, wakampata katika nchi tambarare ya Yeriko; na jeshi lake lote walikuwa wametawanyika na kumwacha.

6-Ndipo wakamkamata mfalme, wakamchukua kwa mfalme wa Babeli huko Ribla; wakatoa hukumu juu yake.

7-Wakawaua wana wa Sedekia mbele ya macho yake, wakampofusha macho Sedekia, wakamfunga kwa pingu, wakamchukua mpaka Babeli.

-Wababeli waliyashinda makabila mawili ya Yuda, na kuwapeleka wengi wao kwenda Babeli ili kuwa watumwa wao.



-Wababeli pia waliuharibu mji wa Yerusalemu.

Tusome 2 Wafalme 25:9-12 & 21

9-Akaiteketeza nyumba ya Bwana, na nyumba ya mfalme; na nyumba zote za Yerusalemu, naam, kila nyumba kubwa aliiteketeza kwa moto.

10-Na jeshi lote la Wakaldayo, waliokuwa pamoja na huyo amiri wa askari walinzi, wakazibomoa kuta za Yerusalemu pande zote.

11-Na mabaki ya watu waliosalia katika mji, nao wale walioasi, na kumkimbilia mfalme wa Babeli, na mabaki ya watu wote wengine, watu hao Nebuzaradani, amiri wa askari walinzi, akawachukua mateka.

12-Lakini huyo amiri wa askari walinzi akawaacha watu walio maskini ili wawe watunza mizabibu na wakulima.

21-Naye mfalme wa Babeli akawapiga, na kuwaua huko Ribla katika nchi ya Hamathi. Hivyo Yuda wakachukuliwa utumwani kutoka nchi yao.

-Je, Wababeli waliuharibu vipi mji wa Yerusalemu?

-Walililiteketeza hekalu.
-Waliteketeza Yerusalemu.

-Waliubomoa ukuta uliozingira mji.

-Mungu aliyaadhibu makabila kumi ya Israeli na mawili ya Yuda kwa sababu hayakuacha njia ya dhambi.

-Baada ya miaka mingi, watu wa Yuda, waliokuwa wakiishi Babeli walimlilia Mungu.

-Walimlilia Mungu, wakamuomba msamaha, na wakatubu dhambi zao kwake.

-Kwa kuwa Mungu ni mwenye rehema, aliruhusu wengi wao warejee Yerusalemu

-Je, watu wa Yuda walifanya nini waliporejea Yerusalemu?

-Walilijenga hekalu tena.
-Waliujenga mji wa Yerusalemu tena.
-Waliujenga ukuta uliozingira mji wa Yerusalemu tena.

-Watu wa Yuda waliorejea Yerusalemu waliitwa jina jipya.

-Je, jina jipya waliloitwa watu wa Yuda waliorejea Yerusalemu ni lipi?
-Wayahudi.

-Ingawaje Wayahudi walimwabudu Mungu, pia waliendelea kuabudu mifano walioifanya.

-Kwa hivyo, Mungu alituma mataifa mawili kuwashinda Wayahudi.

-Je, mataifa mawili ambayo Mungu alituma kuwashinda Wayahudi yalikuwa yapi?
-Wayunani na Warumi.



-Kwanza, Mungu alituma Wayunani kuwashinda Wayahudi.

-Wayunani waliwashinda Wayahudi, na kutawala nchi yao.
-Wayunani pia waliwafundisha Wayahudi lugha ya Kiyuunani.

-Baada ya Wayunani, Mungu aliwatuma Warumi kuwashinda Wayahudi.

-Warumi waliwashinda Wayahudi na kutawala nchi yao.

-Warumi waliwafanya Wayahudi walipe kodi.

-Warumi pia waliwasulubisha Wayahudi wengi kwa kuwaangika kwa misalaba ya mbao.

-Jina la mfalme wa Rumi lilikuwa Kaisari.
-Kaisari aliishi katika mji wa Roma.

-Je, Warumi waliabudu nani?

-Warumi waliabudu mifano mingi.
-Warumi pia waliabudu mfalme wao, Kaisari.

-Wakati huo, kulikuwepo na makundi matatu ya viongozi wa Wayahudi.

-Walikuwa, Waandishi, Mafarisayo na Masadukayo.

-Baadhi ya viongozi wa Wayahudi waliitwa Waandishi.

-Je, Waandishi walikuwa nani?

-Waandishi walikuwa viongozi wa Wayahudi ambao waliyaandika maneno ya Mungu.

-Hapo awali, hakukuwa na vitabu kama tulivyo navyo sasa.

-Watu walipotaka kuandika jambo, waliandika katika karatasi ndefu ambayo ilikunjwa kwa pande zake mbili.

-Musa aliandika maneno ya Mungu katika karatasi ndefu ambayo ilikunjwa kwa pande zake mbili.

-Kwa kuwa watu wengi zaidi walitaka kuyasoma maneno ya Mungu, iliitajika kuyaandika maneno ya Mungu katika makaratasi mapya.

-Wakati wote, Waandishi waliyaandika maneno ya Mungu kwa makaratasi mapya kutoka kwa yale ya kitambo.

-Kwa sababu Waandishi waliyaandika maneno ya Mungu wakati wote, walijawa na kiburi sana.

-Kwa sababu Waandishi waliyaandika maneno ya Mungu wakati wote, waliamini kuwa waliyaelewa.

-Je, kuandika tu maneno ya Mungu, kutakufanya uyaelewe?
-La.

-Kwa sababu Waandishi waliyaandika maneno ya Mungu



wakati wote, waliamini kuwa hawakuwa na dhambi.

-Je, kuandika tu maneno ya Mungu, kutakufanya usiwe na dhambi?

-La.
-Waandishi wengi hawakumwamini Mungu.

-Baadhi ya viongozi wengine wa Wayahudi waliitwa Mafarisayo.

-Je, Mafarisayo walikuwa nani?

-Mafarisayo walikuwa viongozi wa Wayahudi ambao waliyafundisha maneno ya Mungu.

-Mafarisayo pia waliwafundisha Wayahudi sheria za Mungu.

-Kwa kuongezea, Mafarisayo walitunga sheria zao ambazo waliwafundisha Wayahudi.

-Mafarisayo waliamini kuwa walitii sheria zote za Mungu.

-Je, kuna yeyote anayeweza kutii sheria zote za Mungu?
-La.

-Kwa sababu Mafarisayo walifundisha maneno ya Mungu wakati wote, walijawa na kiburi sana.

-Kwa sababu Mafarisayo walifundisha maneno ya Mungu

wakati wote, waliamini kuwa waliyaelewa.

-Je, kufundisha tu maneno ya Mungu, kutakufanya uyaelewe?
-La.

-Kwa sababu Mafarisayo walifundisha maneno ya Mungu wakati wote, waliamini kuwa hawakuwa na dhambi.

-Je, kufundisha tu maneno ya Mungu, kutakufanya usiwe na dhambi?

-La.
-Wengi wa Mafarisayo hawakumwamini Mungu.

-Baadhi ya viongozi wengine wa Wayahudi waliitwa Masadukayo.

-Je, Masadukayo walikuwa nani?

-Masadukayo walikuwa viongozi wa Wayahudi ambao walikuwa matajiri na ambao walilinda hekalu.

-Kwa sababu Masadukayo walikuwa matajiri na walilinda hekalu, walijawa na kiburi sana.

-Kwa sababu Masadukayo walikuwa na pesa nyingi, waliamini kuwa hawakuwa na dhambi.

-Je, kuwa na pesa nyingi kutakufanya usiwe na dhambi?



-La.
-Wengi wa Masadukayo hawakumwamini Mungu.

-Wakati huo, wayahudi walijenga manyumba ambayo waliyaita Masinagogi.

-Je, Masinagogi yalikuwa nini?

-Masinagogi yalikuwa manyumba ambayo wayahudi walikutana ili kusoma na kujadili maandishi ya Musa.

-Wayahudi walijenga Masinagogi katika miji yao yote.

-Katika siku ya mwisho ya wiki, Wayahudi wangeenda katika Masinagogi ili kusikiliza maandishi ya Musa.

-Wakati mwingi, watu wangeelezea maandishi ya Musa.

-Lakini kwa sababu watu hawakumwamini Mungu, maelezo yao kuhusu maandishi ya Musa hayakuwa sawa.

-Wakati huo, Wayahudi wengi hawakumwamini Mungu.

-Je, wakati huo, kulikuwepo na Wayahudi waliomwamini Mungu?

-Ndiyo.
-Kulikuwepo na wachache waliomwamini Mungu.

-Hawa Wayahudi walikuwa wakimsubiri mwokozi.